

**Uchunguzi wa Kidrama wa Riwaya ya Kiswahili na
Maendeleo ya Fasihi Afrika Mashariki: *Unaitwa Nani?* ya
K.W. Wamitila**

Collins Kenga Mumbo
Chuo Kikuu cha Moi, Kenya

Ikisiri

Katika makala haya ninachunguza namna dayalojia ya kidrama inavyotumika katika riwaya za kisasa za Kiswahili kama mbinu mojawapo ya kuwasilisha fikra na mawazo katika kazi ya fasihi; mintarafu riwaya ya *Unaitwa nani?* ya Wamitila. Baadhi ya riwaya za Kiswahili hasa zile zilizoandikwa mwishoni mwa karne ya 20 na mwanzoni mwa karne ya 21 zimekuwa zikitumia fani mbalimbali za kiusasa-baadaye katika fasihi jarabati, msisitizo ukiwa kwenye matumizi ya fantasia ili kuwasilisha ujumbe. Katika uchunguzi huu nimejikita katika riwaya ya *Unaitwa nani?* nikitathmini matumizi ya fani ya dayalojia au lugha ya majibizano kama ilivyotumika katika riwaya kwa minajili ya kuwasilisha fikra. Nimetathmini lugha ya majibizano na usemezano kama inavyobainika katika *Unaitwa nani?* Mijadala mbalimbali inayojitokeza na inavyoendelezwa kuhusiana na suala la kijinsia imezingatiwa kwa makini. Hatimaye kazi hii imekadiria mchango wa riwaya za kiusasa - baadaye katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kwa jumla na hususan katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika. Uchunguzi huu umeongozwa na nadharia ya usemezano ya Mikhail Bakhtin.

Maneno Muhimu: Drama, Dayalojia, Riwaya, Usemezano, *Jarabati*.

Utangulizi

Unapozungumzia riwaya jambo la msingi unalopaswa kulizingatia ni kwamba riwaya ni hadithi, na hadithi hiyo inahusu uzoefu wa maisha ya watu, iwe ya kubuni au iwe inasimulia matukio ya kihistoria bado inaakisi maisha ya wanadamu na mazingira yao. Katika kujadili dhana ya riwaya nataka kuanza kwa kurejelea mawazo ya Edward Morgan Foster 1927 na kurejelewa katika toleo la kielektroniki la mwaka 2002. Japo ni mawazo ya zamani, mwangwi wake bado wasikika hadi leo. Forster alipokuwa amelikwa kutoa mhadhara elekezi katika

chuo cha Trinity cha Chuo Kikuu cha Cambridge Uingereza, kama mwandishi wa riwaya wakati ambapo riwaya yake maarufu *A Passage to India*, ilikuwa imechapishwa. Alitoa msururu wa mihadhara minane ambayo baadaye ilikuja kuchapishwa kama kitabu: *Aspects of the Novel*. Forster katika kujadili dhana ya riwaya alitumia mifano ya watu watatu;

- a) Alisema ukimuuliza mtu fulani kazi ya riwaya ni nini? Atakujibu, “sijui - riwaya ni riwaya tu, husimulia hadithi”.
- b) Mtu wa pili ukimuuliza swali hilo hilo atakwambia, “Bila shaka riwaya husimulia hadithi. Na siitaki riwaya hiyo kama haiwezi kusimulia hadithi. Unaweza kuchukua sanaa yako, unaweza kuchukua fasihi yako na unaweza kuchukua muziki wako, lakini unipe hadithi nzuri. Nataka hadithi iwe hadithi”.
- c) Hatimaye mtu wa tatu anaweza kujibu riwaya lazima isimulie hadithi.

Mjadala huo unatubainishia umuhimu wa hadithi katika riwaya. Mwishoni Forster, E.M. alisema kwamba yeye angekubaliana na jawabu la mtu wa pili, ya kwamba riwaya lazima isimulie hadithi, na si hadithi tu bali hadithi nzuri. Kutokana na jawabu hilo akaifafanua riwaya kama, masimulizi juu ya matukio yaliyopangwa kama yalivyotokea kiwakati. Mara nyingi kufaulu kwa mtunzi wa hadithi kunategemea uwezo wake wa kubuni na kupanga masimulizi

Nikiwaangazia Njogu na Chimera (1999) wameelezea riwaya kama, “utungo mrefu wa kubuni na wenye ploti uliotumia lugha ya nathari. Lakini ploti ni nini? Ploti inahusu maingiliano na mazvano ya vitushi. Yaani, ploti ni jinsi vitushi katika kazi ya sanaa vinavyoingiliana na kuzuana au kusababishana” Naye Wamitila anasema, “riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha. Lakini urefu wa kutosha ni upi? Riwaya inapaswa kuwa na msuko uliojengeka vizuri na ambao unaonyesha vitushi mbalimbali. Aghalabu wahusika katika riwaya huwa wengi na walioendelezwa kwa kina. Kazi yenyewe huchukua muda mrefu na mandhari huwa na mchango mkubwa kuliko ilivyo katika novela na hadithi fupi.

Ni bayana kwamba ufafanuzi wa riwaya kwa mujibu wa wanafasihi hawa unasisitiza suala la ploti au mshikamano na mfumano wa vitushi ufaao. Ni muhimu kutambua ya kwamba si riwaya zote zinazojifunga kwenye ploti, hasa zile ambazo zimeandikwa zikizingatia mitindo ya fasihi ya kiusasa baadaye. Kazi nyingi zilizotungwa kwa kuzingatia nadharia za kiusasa- baadaye kama vile *Nagona* na *Mzingile* za E. Kezilahabi, *Dunia yao*, *Nyuso za mwanamke* na *Mkamandume* za Said A. Mohamed, *Musaleo*, *Harufu ya Mapera* na *Bina-Adamu* za K. W. Wamitila, hazijajikita kwenye ploti kama ilivyofafanuliwa na Aristotle. Hata hivyo nataka kutaja hapa ya kwamba kati ya wanafasihi niliowanukuu hapo juu:

Njogu akiandika na Wafula amelitambua suala hilo ya kwamba riwaya ya kiusasa baadaye haizingatii ploti, pale wanapokiri kwamba "... muwala na mshikamano wa kazi ya fasihi kama ilivyozowewa na mapokeo si muhimu tena. Nadharia hizi zinashikilia kwamba kazi za fasihi hujengwa kutokana mchangamano wa tajriba ama uzoefu." Kwa hivyo riwaya ni hadithi inayosimuliwa kwa kipindi kirefu na inayojumuisha visa na matukio yanayohusu uzoefu wa maisha ya watu katika jamii, viwe vya kindoto au vya kiuhalisia.

Kwa upande mwingine ninapozungumzia drama ninarejelea mtungo wa kisanaa unaotumia lugha ya majibizano baina ya wahusika katika kusawiri mawazo na migogoro inayoikabili jamii kwa njia ya utendaji. Hatima ya drama ni kuigizwa mbele ya hadhira. Ile hali ya utendaji au uigizaji unaoshuhudiwa na watu ndio msingi wa drama. Banks R. (1985) anasema kwamba drama inajumuisha uwakilishaji wa maisha halisi ya watu, na ambao unaweza kuwa utungo wa kinathari au kishairi lakini unapowasilishwa jukwaani kwa njia ya matendo na maongezi inakuwa drama. Maelezo haya ya Banks ni muhimu kwa makala haya kwa sababu yanadokeza kwamba, hata kazi za kinathari zinapowasilishwa kwa njia ya utendaji na lugha ya majibizano inaweza kuwa drama. Kwa hivyo drama iko katika njia ya uwasilishaji wa kimatendo na majibizano.

Historia ya Riwaya ya Kiswahili

Fasihi andishi kwa Kiswahili ina historia ndefu kama ilivyo historia ya maandishi yenyewe Afrika Mashariki. Inakisiwa ya kwamba fasihi ya Kiswahili ilianza karne ya 10 wakati maandishi ya Kiarabu yalipofika kwa mara ya kwanza katika pwani ya Afrika Mashariki. Ulaya Magharibi riwaya ilianza kutumika katika karne ya 14 na 15 baada ya uvumbuzi wa karatasi. Utanzu wa mwanzo wa fasihi ulioshika Afrika Mashariki kabla ya majilio ya wakoloni wa Kiarabu na Kizungu pamoja na wamishonari ni ushairi kwani unafungamana na nyimbo za kimasimulizi. Asili ya fasihi andishi inatokana na fasihi simulizi ya Waafrika. Tanzu za awali kabisa za fasihi andishi zinahusiana moja kwa moja na fasihi simulizi kama vile mashairi, nyimbo, ngano, vitendawili, visasili, visakale, methali na ngoma.

Riwaya ya kwanza kuwahi kuandikwa moja kwa moja kwa Kiswahili bila kutafsiriwa kutoka lugha nyingine ni *Uhuru wa watumwa* iliyoandikwa na James Mbotela na kuchapishwa mwaka 1934. Kimaudhui na kifani riwaya hii inaakisi utamaduni wa Kiafrika. Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* uandishi wake ulichukua mfumo wa kitawasifu. Katika riwaya hii Waarabu wanalaumiwa kwa kuendeleza biashara ya utumwa Afrika Mashariki ilhali wakoloni wa Kimagharibi wanasifiwa kwa kusitisha biashara ya utumwa na kuwapa watumwa uhuru. Walipowasili wamishonari na walowezi Afrika Mashariki, ngano kadha zilitafsiriwa na zikawa ndio msingi wa utunzi wa riwaya kwa mujibu wa vigezo

vya Ulaya Magharibi kama vile *Mazungumzo ya Alfu Lela Ulela* juzuu 1-4, zilizotafsiriwa na Brenn na kuhaririwa na Johnson. Tafsiri nyingine za hadithi za Kimagharibi; *Mashimo ya Mfalme Suleiman* na Haggard *Kisima chenye hazina* ya Stevenson, *Safari za Guliva*, Swift na *Hadithi za Esopo*. Hata hivyo wapo wamishonari wengine ambao walikusanya ngano za Kiafrika na kuzichapisha kama masimulizi ya kiriwaya, kama alivyofanya Askofu Edward Steere na *Swahili tales as told by the natives of Zanzibar*.

Baadaye waandishi kama vile Shaaban Robert waliibuka na riwaya kama zao: *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguze*. Shaaban Robert aliukashifu utawala wa kikoloni na kuonyesha mgogoro uliokuwepo baina ya wakoloni na Waafrika, lakini alifanya hivyo kwa kutumia tashtiti na mafumbo katika kazi zake. Waandishi wengine waliojitokeza katika kipindi hiki ni pamoja na Mohamed Said Abdalla na riwaya zake za kiupelelezi, baada ya uhuru wakaingia waandishi wasomi kama kina Kezilahabi, Katama Mkangi, Said A. Mohamed, Rocha Chimera, Wamitila na wengineo. Riwaya ya Kiswahili hivi leo imefika upeo wa juu kimaendeleo kwani tumeshuhudia majaribio ya kimtindo na kinadharia.

Uhakiki wa fasihi andishi ulikuwa umekwama katika fani na maudhui kwa muda mrefu, lakini katika miongo hii miwili iliyopita uchanganuzi wa fasihi kwa jumla umekua na kupanuka, ukiangazia mawanda mapana, mengi na mapya yakiwemo ya kifalsafa, kinadharia na hata ya teknolojia ya habari na mawasiliano kama inavyodhihirika kupitia kwa kazi kama vile *Nagona* na *Mzingile* za E.Kezilahabi, *Walenisi* ya K.Mkangi na *Babu alipofufuka* ya S.A.Mohamed na nyinginezo. Dhana za miaka ya 1970 kwamba fasihi ya Kiswahili ni fasihi ya watu wachache – Waswahili wanaoishi pwani ya Afrika Mashariki hazina nafasi tena katika fasihi ya leo, kwani fasihi ya Kiswahili imeweza kupanuka kadri matumizi ya lugha yake yanavyokua hadi kufikia kiwango cha fasihi ya kilimwengu. Hali hii imebainika wazi kutokana na kazi za fasihi hususan riwaya za hali ya juu zinazoandikwa na kuchapishwa kwa kasi mno katika kipindi cha mwishoni mwa karne ya 20 na mwanzoni mwa karne ya 21, zikijikita katika fani anuwai za fasihi ikiwemo ile ya fasihi jarabati na kujadili masuala ya kinadharia pamoja na ya kifalsafa. Ni katika mwelekeo huo ndipo ninachunguza matumizi ya fani ya kidrama au dayalojia katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili ambao ni mkondo mmojawapo wa kiusasa-baadaye, katika mwingiliano matini.

Kwa Nini Unaitwa Nani?

Riwaya ya *Unaitwa Nani?* ya Wamitila, K. W. ni riwaya iliyoandikwa na kuchapishwa mwaka 2008 kwa mara ya kwanza na kampuni ya Vide-Muwa. Ni miongoni mwa riwaya ambazo zimetumia mbinu ya dayalojia kwa mapana, licha ya kwamba zipo riwaya nyingine ambazo zimetumia mbinu hiyo kama vile, *Haini* ya Shafi, A. na *Dunia Yao* ya Said A. Mohamed. Riwaya ya *Unaitwa Nani?* imesimikwa kwenye matini ya kidrama inayotumia dayalojia ama usemezano

katika kuwasilisha mawazo yake. Ujumbe umewasilishwa kwa lugha ya majibizano ya kidrama, maarufu kama dayalojia. Mbali na matumizi ya dayalojia, riwaya hii vile vile inaonyesha matumizi ya mwingiliano wa sauti mbali mbali katika dayalojia zake kama inavyojitokeza katika nadharia ya usemezano ya Mikhail Bakhtin. Kwa hivyo riwaya hii ya *Unaitwa Nani?* ni kielelezo cha matumizi ya fani ya dayalojia katika ngazi ya usemezano ili kuwasilisha mawazo yake kwa wasomaji.

Matini ya Kidrama

Ninapozungumzia matini ya kidrama hapa ninarejelea ile lugha ya kimajibizano baina ya wahusika. Ninaashiria maneno ambayo yamelengwa kuwasilishwa na wahusika; kuigizwa au kutendwa mbele ya hadhira. Maneno ambayo yamesheheni utendaji. Maneno haya yanasababisha vipi utendaji? Yanaelekeza kile cha kusemwa; kitasemwa namna gani; kwa nani; katika muktadha upi; kwa kutumia matendo yapi na mahali gani. Ni kutokana na mantiki haya ndipo naweza kufafanua matini ya kidrama kama maneno yaliyoundwa ili yafasiriwe na waelekezi pamoja na waandalizi wa sanaa za maonyesho ambao baadaye watawasilisha igizo hilo mbele ya hadhira yao. Matini ya kidrama ina vipengele viwili muhimu cha kwanza ni dayalojia inayojengwa na wahusika na pili maelekezo ya utendaji. Katika uchunguzi wa kidrama wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* nimezingatia jumla ya vipengele vitatu vikuu; yaani kauli za majibizano, maelekezo ya utendaji na mandhari ya utendaji.

Mwingiliano Matini na Usemezano

Katika kuchunguza riwaya ya *Unaitwa Nani?* kidrama nimejifunga na mtindo wa dayalojia kwa mujibu wa nadharia ya usemezano ya Mikhail M. Bakhtin (1895-1975). Bakhtin anaiona kazi ya fasihi kama jukwaa changamano la mtagusano wa matini. Anasema kuwa uhusiano huu wa matini ni wa kiusemezano baina ya sauti mbalimbali za usemi. Uhusiano huu wa lugha ndio Julia Kristeva alioelezea kama mwingiliano matini. Istilahi ya “Mwingiliano matini” ilibuniwa na kutumiwa kwa mara ya kwanza na Julia Kristeva katika insha yake, “Word, Dialogue and Novel” 1966 na baadaye katika “The Bounded Texts” akirejelea dhana hii ya Mikhail Bakhtin ya kiini au maana ya matini za kifasihi; kwamba kila neno katika riwaya ni sehemu ya neno jingine, yaani yanahusiana na kuingiliana. Kwa hivyo dhana na nadharia ya mwingiliano matini inahusishwa na Kristeva, licha ya kwamba aliathiriwa pakubwa na mawazo ya Mikhail Bakhtin.

Kulingana na Bakhtin kazi ya fasihi inashirikisha sauti mbalimbali na mazungumzo ya kila siku ambayo yako nje ya matini rasmi. Uzungumzi binafsi unapowachwa unaweza kufungia nje dayalojia na uhuru. Katika usemezano siku zote kuna nafasi ya majadiliano kwani uchunguzi hufuata mwelekeo wa asili ya maisha, msisitizo ukiwa kwenye maoni kuliko ukweli. Kwa mfano katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, mwandishi anarejelea mtazamo wa Sigmund Freud kuhusu

suala la mwanamke na jinsia, kwamba Freud aliwaona wanawake kama viumbe dhaifu na wanyonge katika nyanja zote, na jinsi mwandishi anavyohusisha asili ya mawazo hayo na mwanafalsafa mkongwe wa Kiyunani, Aristotle pamoja na Friedrich Nietzsche. Hali hii inatupa picha ya wanafalsafa mbalimbali walioishi katika vipindi tofauti wakijadili suala lile lile la jinsia na kila mmoja akitoa maoni yake, ambayo yanalingana kwa kiasi kikubwa. Mbali na hayo mwandishi anarejelea michezo ya watoto kama vile, “nyamanyama nyamanyama” katika kukuza usemezano. Sifa nyingine za kiusemezano zinazojitokeza katika riwaya hii ni pamoja na ububu, ubaradhuli, upumbavu, ucheshi, kujitweza na kujitwaza katika wahusika wakuu, Mwanamke na Mwanamume.

Katika muktadha wa mwingiliano matini, Wamitila amejumuisha takribani tanzu zote za fasihi, hali ambayo inapelekea kuwepo kwa mwingiliano tanzu ndani ya mwingiliano matini. Ametumia visa vya fasihi simulizi, kwa mfano kile kisa cha wanawake wa jamii ya Fiote wanaoishi nchini Angola ambao wanawake wao walikuwa wafinyanzi maarufu wa bunguu. Wanawake hawa walitumia usanii wao kuwasilisha hisia zao za ndani kuhusu waume zao (Uk. 25). Kisa cha Wangu wa Makeri ambacho kinatajwa tu, masimulizi ya kisa cha Nyalgondho aliyekuwa mvuvi maskini na Mwanamke wa ziwa Sango (uk. 72-75). Hadithi hii inafundisha kwamba ukipata mali usifanye kiburi na kusahau ulikotoka kama alivyofanya Nyalgondho, kwani majuto ni mjukuu huja baadaye. Wamitila vile vile ametumia vipera vya semi na nyimbo za fasihi simulizi. Kwa upande wa fasihi andishi mbali na tamthilia, amejumuisha tanzu za ushairi na hadithi fupi, zote zikisukwa kwa ufundi na ubunifu ili kuwasilisha kazi ya riwaya. Pamoja na tanzu za kifasihi, kazi hii vile vile imetumia tanzu za kitaaluma kama vile utabibu, historia, saikolojia na sanaa. Kwa hivyo ni kazi ya kifasihi ambayo imeundwa kwa misingi ya kiusemezano kwa kujikita katika matumizi ya mtindo wa mwingiliano matini ili kujadili mawazo ambayo mwandishi anataka wasomaji wake kuyadadisi na kujinasibisha nayo – suala la jinsia; taswira ya mwanamke na mwanamume katika jamii.

Mbinu ya Dayalojia

Kwa mujibu wa makala haya, dayalojia ni mtindo wa lugha ya majibizano ambao unatumika sana katika drama au tamthilia - ni kauli za majibizano. Lugha ya majibizano ndiyo nguzo kuu ya utunzi wa tamthilia na michezo ya kuigiza kwa sababu ndio wenye kuongoza utendaji. Sifa kuu ya majibizano au dayalojia ya kidrama ni sentensi fupi fupi kama ilivyo katika ushairi. Lengo la kutumia sentensi fupi katika drama ni kurahisisha uigizaji jukwaani, kwani mchezo wa kuigiza madhumuni yake ni kuwasilishwa kiutendaji mbele ya hadhira na wala si kusomwa tu. Dayalojia dhima yake si kuwasilisha ujumbe pekee, bali inatekeleza majukumu mengine kama vile kubainisha taswira mbalimbali, kubuni na kuelekeza miondoko jukwaani na kujenga ulimwengu wa matukio katika uigizaji. Katika riwaya ya *Unaitwa nani?* dayalojia imetumika kwa kiwango kikubwa

katika kujenga na kukuza maudhui. Riwaya hii inaadadisi suala la jinsia na utambulisho katika jamii. Riwaya ya *Unaitwa Nani?* imetawaliwa na dayalojia ya kiusemblezani. Kauli hizi za majibizano zinabainisha sifa mbalimbali za kiusemblezani.

Mfano 1

Palikuwa na kimya kirefu kisha harakati za hapa na pale. Sijui walikuwa wakifanya nini? Nilijitahidi kuyafungua macho yangu tena japo kwa shida. Nikashindwa. Sasa macho yangu hayawezi kunifaa. Labda nijaribu kinywa. Nilijitahidi kupeleka ulimi wangu mbele na kuilamba midomo niliyohisi ikiwa mikavu kama ya mla maembe mabichi. Ulimi uliniganda kinywani kama mtu aliyedungwa sindano ya kung'olewa jino (*hivi mimi nasubiri kung'olewa nini?*).

Nilijitahidi kuikutanisha midomo yangu miwili niliyohisi mizito ajabu kama mtu aliyemwa na mavu, au mrina asali ambaye kwa pupa anauma sega la nyuki na kufumwa na usena wa nyuki mwenye hasira, lakini sikufanikiwa. Nilijaribu kuipitisha ulimi wangu juu ya midomo yenyewe na kuhisi ugwadu fulani. Lazima nilikuwa nikifanya kama mtu anayebabatiza maneno asiyoyajua.

“Nilidhani anajaribu kuongea”

“Kuongea?”

“Ehhh!”

(Kicheko kingine)

“Kuongea gani?”

“Hawezi!”

“Tumempa *sedatives*. Hawezi!”

“Huioni midomo inavyocheza tu...”

“Ni kama amepoteza fahamu!”

“Inaelekea!”

“Ataipata lakini?”

“Ndivyo kama ana bahati”

“Ehhh?”

“Wengine huipata!”

“Na wengine?”

“Wanakufa alaa! Unadhani mwanamke kufa ni nini? Wangapi wamekufa nchi hii?”

(Kicheko kingine)

(Uk. 9-10)

Mazungumzo haya ni baina ya matabibu ambao mgonjwa wao, Mwanamke alikuwa amepoteza fahamu wakidhani hasikii chochote, kumbe alikuwa akifuatilia kila kitu walichokuwa wakisema. Sehemu ya mwanzo ya mazungumzo haya inaonyesha hali taabani aliyokuwa mgonjwa huyo, akijitahidi kujaribu kuongea lakini ikamwia vigumu kutokana na maumivu aliyohisi. Maelezo hayo vile vile yanajitokeza kama maelekezo ya jukwaa kama ilivyo katika drama. Maelekezo ya namna hii huwa yanaongoza uigizaji ama utendaji. Maneno yanayofuata, ni mazungumzo au dayalojia baina ya matabibu kwenye wodi ya hospitali yakidokezea ubaradhuli wa matabibu hao dhidi ya mwanamke. Katika sehemu hii usemezano baina ya wahusika mbalimbali na kwenye muktadha huu wakiwa madaktari, tunaonyeshwa namna ambavyo mwanamke anadharauliwa, kudhalilishwa na kuonekana si chochote si lolote. Wanafikia kiwango cha kusema kwamba mwanamke kufariki si jambo kubwa katika nchi yao kwani wengi wameshafariki, kwa hivyo hata yeye anaweza kufa tu, na hilo haliwezi kuwashtua wao.

Mfano 2:

Nilijitahidi kwa nguvu zangu zote. Maumivu yalikuwa makali lakini sikutaka kushindwa mara zilizotangulia. Ilikuwa lazima nitamke kitu mara hii ...

“Mwana wa nani?”

“Mwa...ana..”

“Wa nanii..i..i nauliza” (Kwa sauti kubwa sana)

“Eeh, smaaa!”

“Mwa...ana...m..”

“Mwanamume gani?”

“Mwana...mke..”

“Anasema nini huyu mwanamke?”

“Ni vigumu kujua!”

“Hatutapoteza muda hapa unasikia? Jina lako ni nani?”

“Yaani unaitwa nani?”

“Mwana..ana..mke! Mwanamke!”

Nilifurahi kuwa hatimaye nimefanikiwa kulitaja jina langu. Bila shaka watafurahi baada ya kunisumbua kwa muda wakitaka niwaeleze mimi ni nani. (kimya. Baada ya muda kicheko.) Kicheko hicho kiliendelea kwa muda. Nilijua wananicheka mimi. Lakini nilihisi kuwa nimeutua mzigo

mzito mabegani, kitu kama gunia la maharagwe. Nimewaeleza mimi ni nani?

“Ati unasema unaitwa nani?”

“Mwanamke!”

“Hilo tunajua! Alaaa!”

“Unadhani hatuna macho?”

“Eeh, semaa!”

“Hivi vilivyoko usoni unadhani nini? Globu?”

“Tuambie jina lako?”

“J...i...i...na, unasikia?”

“Mwanamke!”

“Tunachotaka ni jina ehh... Tunataka jina kama la wanawake tunaowajua. Na yapo mengi ya aina hiyo! Majina wanayopewa wanawake kama Hawa, Jezebeli, Delilah au Pandora....

(Uk 14-15)

Katika mfano huu dayalojia iliyopo inahusu utambulisho wa mwanamke. Mjadala wa utambulisho unaendelezwa na mhusika mkuu Mwanamke kwa upande mmoja na matabibu kwa upande wa pili. Dhana ya jina kama kitambulisho cha mtu binafsi na kitambulisho cha ukoo au jamii imebainika kutokana na mazungumzo ya madaktari ambao ni wa jinsia ya kiume. Mwandishi, kupitia kwa mazungumzo ya madaktari anatuonyesha ya kwamba jina ni kitambulisho cha jinsia, kwa hivyo matabibu hawa wanataka Mwanamke awatajije jina ambalo linatambulika kuwa la kike; “Majina wanayopewa wanawake kama Hawa, Jezebel, Delilah au Pandora.” Madaktari wanataka jina ambalo linaweza kumtambulisha mtu binafsi na jinsia yake, jina linaloweza kumfanya mtu kufahamu wasifu au tabia ya mtu. Wanaamini kwamba jina lina uwezo mkubwa.

Mjadala mwingine unaendelezwa na mhusika Mwanamke, ambaye kutokana na masaibu yaliyomfika mpaka akalazwa hospitalini yalimwathiri vibaya kiasi cha kupoteza kumbukizi zake. Hali hii ilimfanya kutoweza kukumbuka hata jina lake, hata hivyo aliweza tu kukumbuka jinsia yake - ya kwamba ni mwanamke. Mwanamke huyu anahisi kwamba mtu kutambua jinsia yake si jambo dogo, isitoshe anaona ya kwamba mtu kutambua jinsia yake ni njia mojawapo ya kujitambulisha. Uzungumzi huu unamhusu mtu na nafsi yake, unathibitisha kwamba uwezo wa mtu kutambua jinsia yake ni hatua muhimu katika utambulisho wake.

Mbali na suala la utambulisho Mwanamke anajadiliana na nafsi yake kuhusu namna ambavyo wanaume wanamdunisha kwa kukosa kwenda shule na badala

yake kukimbilia kuolewa. Wachache walioogopa maisha ya vijijini walikimbilia mjini na kujitumbukiza kwenye biashara ya ukahaba ili kupata pesa kwa urahisi na wengine wakaishia katika matangazo ya biashara. Dhana hii ya woga na udhaifu inamsumbua sana Mwanamke kiasi kwamba anaisaka nafsi yake; “Je, hivi nimeumbwa na woga fulani unaonizuia kusema yaliyonikaa moyoni au mwenyewe nimezongomezwa kwenye maisha ya woga au maisha yenyewe ni mkufu mzima uliojaa shanga za hofu na woga? ... Je, ni maumbile yangu au ni udhaifu wangu kama kiumbe? Kwanza hata nani aliyesema kuwa mimi kama kiumbe ni dhaifu?” Katika kujisaka na kujisaili, mwanamke amechukua nafasi muhimu katika jitihada za kujinyanyua na kubadili taswira hasi inayomkabili katika jamii. Mjadala huu ni chemchemi maridhawa katika harakati za kumkomboa mwanamke kimawazo na kumwezesha kumtambua na kuchukua nafasi yake kikamilifu katika jamii.

Mfano 3

“Ha..wa eee..h...i..vi...umbe...!”

“Ndio maana hata kuongoza hawawezi...!”

“Uongozi hawawezi! Umenikumbusha jambo muhimu!”

“Kweli eeh?”

“Sema!”

Katika imani ya Confucious, Yule msomi wa Uchina, mwanamke kutawala ni kama kuku kuwika alfajiri...!”

“Ile Siku inaharibika kabisa!”

“Kabisa!”

“Ushirikina huo!”

“Ushirikina gani wewe nawe?”

“Lakini nasikia huko Uchina kwenyewe kuna mwanamke aliyetawala..”

(Kicheko kikubwa)

“Kumbe wapo wenye fahamu nzuri?”

“Labda katika fasihi simulizi...!”

“Hizo ni ngano na ngano kama hujui haziaminiwi!”

(Uk. 35)

Katika mfano 3, lugha ya majibizano iliyotumika inabainisha sifa za kumtweza na kumtwaza mwanamke. Usemezano huu unatoa taswira ya udhaifu wa mwanamke hasa kuhusu suala la uongozi na kuendeleza kiburi cha mwanamume. Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mnyonge asiyeweza kutawala wala kuaminika katika ngazi ya uongozi.

Katika mazungumzo ya ‘Ndoa ya Giza’ na ‘Kitumbua’ kwenye riwaya ya *Unaitwa Nani?* mwandishi anadadisi suala la ndoa na utamaduni yanavyotumiwa katika jamii kumnyanyasa mwanamke. Mahali pa mwanamke kwa mujibu wa utamaduni ni jikoni ambapo wanapaswa kukaa na kuwashauri binti zao kuhusu namna ya kuishi kwa lugha ya jikoni, ilhali mwanamume mahali pake ni barazani ambapo hukaa na matumbo yao wakivuta sigara na kusoma magazeti. Mwanamke anatarajiwa kuwa mnyenyekevu kwa mumewe kwa sababu mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba, mfadhili wa maisha ya mwanamke, mwenye kumkinga mwanamke dhidi ya ukatili wa ulimwengu, mwelekezi na mnasihwa wa mwanamke kama inavyoelezwa katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Katika mjadala huu gharama ya mwanamke inakadiriwa kwa mahari anayolipiwa. Mwanamume anashangazwa na jinsi jamii inavyomnadi mwanamke kwa gharama ya mbuzi watatu kama mahari, jambo ambalo linamdundisha mwanamke. Thamani ya mwanamke inapimwa kwa uwezo wake wa kuzaa mtoto. Katika sehemu ya pili ya riwaya ya *Unaitwa Nani?* tunakumbana na Mwanamume ambaye pia ni mgonjwa mahututi, yuko hospitalini amepoteza fahamu. Halikadhalika yeye pia halikumbuki jina lake lakini anachokumbuka ni jinsia yake, kuwa yeye ni Mwanamume.

Mfano 4

Najaribu kukumbuka ilivyokuwa mpaka nikawa katika hali niliyoko sasa lakini siwezi. Ni kama ubongo wangu hauna chochote, umefutwa na uhai kila kitu kama ubao unaofutwa baada ya mwalimu na vitabu vyake kuondoka. Ikiwa wanaweza kuyafuata mawazo yangu mbona hawawezi kujua kuwa siwezi kuelewa ni masaibu gani yalivyopata?

“Sema wewe ni nani?”

“Alaaaa!”

“Unaitwa nani?”

“Mwa.....!”

“Mwaaa nini?”

“Hatuna maji sisi au unamwaa wewe?”

“Mwana...!”

“Wa nani?”

“Jina la mamako?”

“Eh, lugha ya mama unayo?”

“Maana hakuna lugha ya baba!”

“Taja jina la mama!”

“Au nyanyako au mamkwe?”

“Au mkeo!”

(Uk. 134-135)

Mwanamume huyu anasemezana na nafsi yake akishangaa kama kweli hawa watu wanafahamu kinachoendelea katika akili yake, kwa nini basi hakuna ajuaye masaiibu yaliyomfika hadi akafikishwa hospitalini. Suala la utambulisho linarejelewa tena lakini kwa mkondo tofauti. Matabibu katika kusemezana kwao wanadai kwamba mtu anaweza kujitambulisha kupitia kwa jina lake, lugha mama, au jina la mkewe. Mwanamume anaweza kutambulika kutokana na jina la kuukeni yaani jina la mamake mzazi ama nyanyake. Mtu anaweza kujitambulisha kwa kutumia jina la ukoo wa kuume au wa kuke. Matabibu walioko ambao ni wa jinsia ya kike wanamdhalilisha mwanamume.

Katika sehemu hii tunapata taswira ya mwanamume ambayo inakinzana; kwa upande mmoja tunachorewa mwanamume mbaye ni shujaa, jasiri na mwenye nguvu kama simba na upande wa mwingine tunaonyesha mwanamume ambaye ni dhaifu, anapenda kudekezwa na kubembelezw. Mwanamume ambaye ni kama mtoto, anayetaka kubebwa mgongoni na kufanyiwa karibu kila kitu. Mitazamo hii miwili ya mwanamume inatupa sura mbili za mwanamume katika jamii, hata hivyo mtazamo wa kwamba mwanamume ni mtu anayependa kudekezwa huenda usitoe picha halisi ya mambo kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika. Lakini kulingana na nadharia ya usemezano mitazamo yote miwili inaweza kukubalika kwani nadharia hii inazingatia suala la msimamo au maoni badala ya kujifunga na suala la ukweli. Na mtu anapozungumzia ukweli, ukweli huo ni kwa mujibu wa nani? Kwa hivyo mjadala wa jinsia unaendelea.

Kazi hii inahusu maisha ya mwanadamu, yaani mke na mume kama anavyokiri mwandishi wa riwaya hii anapohitimisha kwa kusema kwamba, “Labda itahalisi hadithi mpya ya maisha isimuliwe kwa nafsi ya kwanza wingi, hadithi ya mtazamo wa ndani... Tunaitwa nani? Si hilo tu. Tunajiita nani? Hadithi ya mwanamke na mwanamume. Hadithi ya binadamu.” (Uk. 256) Hatimaye mwandishi anasemezana na wasomaji wake moja kwa moja, na kuwajuza ya kwamba riwaya yake ni hadithi ya maisha ya mwanadamu. Anamalizia kwa kumuuliza kila mtu anaitwa nani? Akiwemo msomaji.

Taksiri ya Riwaya ya *Unaitwa Nani?*

Unaposoma riwaya ya *Unaitwa nani?* utakuta ya kwamba kuna baadhi ya matukio na masimulizi ambayo mwandishi ni kana kwamba ameyalazimisha ama kwa sababu za nadharia au uhariri. Mwandishi wa riwaya hii amejikita katika nadharia ya usemezano kipengele cha mwingiliano matini pamoja na ufeministi. Katika juhudi za kutosheleza mahitaji ya kinadharia baadhi ya visa na matukio yamefanya kutajwatajwa tu, bila ufafanuzi wa kina kuafiki sababu za kutajwa kwake. Jambo ambalo limesababisha utata katika kupata ujumbe uliokusudiwa katika baadhi ya matukio. Kwa mfano kurejelewa kwa historia ya enzi ya mawe

ikifuatiliwa na mchezo wa watoto wa “nyamanyama” na kutajwa kwa mfululizo kwa wanafalsafa Sigmund Freud, Aristotle na Friedrich Nietzsche katika suala la udhaifu wa mwanamke. Madai ya kwamba wanafalsafa wote hao watatu walikuwa na maoni sawa kuhusu udhaifu wa mwanamke ni ya kupotosha wasomaji. Hali ya kuzungumzia udhaifu wa mwanamke katika nyanja zote, bila kubainisha kila mwanafalsafa alichosimamia hasa, na badala yake kuwazungumzia kwa pamoja inatatanisha. Mwanafalsafa mkongwe Aristotle alimweleza mwanamke kama mnyonge na dhaifu ambaye anastahili kuwa chini ya mwanamume, lakini udhaifu wake hauwezi kulinganishwa na ule wa mtumwa. Mawazo haya ya Aristotle yaliendelezwa na Nietzsche. Hata hivyo mawazo ya Nietzsche kuhusu suala la mwanamke yana utata; kwanza yanamtukuza mwanamke na pili yanamdunisha. Baadhi ya wahakiki wa fasihi wanahisi kwamba maoni ya Nietzsche yanayoelekea kumdunisha mwanamke ni tashtiti tu na wala si udhalilishaji halisi. Kwa upande wake Sigmund Freud anaangazia hali ya mwanamke kukosa uume kama udhalilishwaji. Kwa hakika ninachosema hapa ni kwamba, si haki kuzungumzia misimamo ya kifalsafa kwa jumla bila ufafanuzi unaostahili kwa minajili ya kufikia azma yetu ya fani na mtindo katika fasihi.

Hitimisho

Katika makala haya, nimeonyesha jinsi ambavyo riwaya ya *Unaitwa Nani?* imezingatia mtindo wa dayalojia ya mwingilianomatini kwa kujifunga na nadharia ya usemezano ya Mikhail Bakhtin. Wamitila ameweza kukuza na kuendeleza majibizano ya kiusemezano katika ngazi mbalimbali: usemezano kati ya mhusika na nafsi yake; usemezano baina ya wahusika wawili au zaidi; usemezano kuhusu dhana tofauti tofauti kama vile, jinsia, jina na utambulisho, sanaa, nadharia au falsafa; usemezano baina ya wahusika na wasomaji; na hatimaye usemezano kati ya mwandishi na wasomaji wake moja kwa moja. Riwaya hii, kwa kiasi kikubwa, imetumia nadharia ya usemezano, hususan mazungumzo ya kidayalojia katika kuwasilisha ujumbe kuhusu suala la jinsia na maisha ya mwanadamu kwa jumla.

Kupitia kwa mijadala nafsia ya wahusika wakuu Mwanamke na Mwanamume na mazungumzo baina ya wahusika wengine, suala la jinsia na utambulisho limechunguzwa katika jamii, kwa kuakisi mitazamo tofauti tofauti. Kwa mfano namna ambavyo baadhi ya wanaume wakiwemo matabibu na wanafalsafa wanavyomchukulia mwanamke kuwa ni kiumbe dhaifu, ilhali wanawake nao wanamdharau mwanamume. Usemezano juu ya utambulisho umebainisha mitazamo anuwai kuhusu jina. Jina linaweza kuchukuliwa kama kitambulisho cha mtu binafsi, ukoo, sifa au tabia ya mtu ama jinsia yake. Kwa upande mwingine mtu anaweza kujitambulisha kupitia jinsia, lugha mama, kupitia kwa jina la mamake au jina la mkewe kama ni mwanamume au hata jina la nyanyake. Kwa hivyo matini hii ya kidayalojia inatubainishia usemezano kuhusu masuala mbalimbali yanayoathiri maisha ya mwanadamu.

Licha ya taksiri ambazo zimejitokeza katika riwaya hii, *Unaitwa Nani?* bado imeakisi kukua na kuendelea kwa fasihi ya Kiswahili Afrika ya Mashariki. Hii ni kazi ya riwaya ya kimajaribio kuhusu matumizi ya nadharia za kiusasa baadaye katika fasihi. Riwaya hii pamoja na nyingine nilizotangulia kuzitaja awali kama vile *Nagona*, *Mzingile*, *Babu Alipofufuka*, *Dunia Yao* miongoni mwa nyingine, zimetoa mchango mkubwa katika fasihi ya majaribio na kuimarisha fasihi ya Kiswahili hadi kufikia kiwango cha fasihi ya kimataifa katika kipindi hiki cha mwongo mmoja na nusu cha karne ya 21.

Marejeleo

- Banks, R. A. (1985). *Drama and Theatre Arts*. London: Hodder & Stoughton.
- Bray, J., Gibbons, A., & McHale, B. (Eds.) (2012). *Routledge Companion to Experimental Literature*. New York and Oxon: USA and Canada.
- Forster, E. M. (2002). *Aspects of the Novel*. New York: Rosetta Books.
- Hale, J. D. (2006). *The Novel: An Anthology of Criticism and Theory 1900-2000*. Malden: USA, Oxford and Victoria: Blackwell.
- Holquist, M. (Ed.). (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays by M. M. Bakhtin*. University of Texas.
- Kezilahabi, E. (2011). *Nagona*. Nairobi: Toleo la Vide-Muwa.
- Kezilahabi, E. (2011). *Mzingile*. Nairobi: Toleo la Vide-Muwa.
- Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*, Edited by Leon S. Roudiez. New York: Columbia UP.
- Mohamed, S. A. (2013). *Mkamandume*. Nairobi: Sasa Sema, Longhorn.
- Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Sasa Sema, Longhorn.
- Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford UP, East Africa Ltd.
- Njogu, K., & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Robert, S. (1968). *Kufikirika*. Nairobi: Nelson Brothers.
- Robert, S. (1952). *Adili na Nduguze*. Nairobi: Nelson Brothers.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Nelson Brothers.
- Rollins, J. (1983). *A History of Swahili Prose, Part 1: From Earliest Times to End of the Nineteenth Century*. Brill: Leiden E.J.
- Sim, S. (Ed.). (2005). *The Routledge Companion to Postmodernism, Second Edition*. London & New York: Routledge Taylor & Francis.
- Wafula, R., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2012). *Harufu ya Mapera*. Nairobi: Videmuwa.

- Wamitila, K. W. (2008). *Unaitwa Nani?* Nairobi: Videmuwa.
- Wamitila, K. W. (2004). *Musaleo*. Nairobi: Videmuwa.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.
- Wamitila, K. W. (2002). *Bina Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Willis, M., & Shepherd, S. (2002). *Studying Plays, Second Edition*. London: Hodder.

